JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## KUSITISHA KWA MUDA LESENI YA HUDUMA ZA MAUDHUI MTANDAONI ILIYOTOLEWA KWA VAPPER TECH LIMITED (JAMIIFORUMS)

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), inatoa taarifa kwa Umma kuwa, mnamo tarehe 04 Septemba 2025, JamiiForums kupitia jukwaa lake na akaunti zake za mitandao ya kijamii ilichapisha maudhui ya kupotosha Umma, kukashifu na kudhalilisha Serikali na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinyume na Kanuni za Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020 na Marekebisho yake ya mwaka 2022 na 2025.

Pamoja na kukiuka Kanuni, maudhui hayo yanakinzana na utamaduni, mila na desturi za Kitanzania, jambo ambalo linaathiri umoja, amani na mshikamano wa kitaifa, na kuharibu taswira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura 306, TCRA IMESITISHA kwa muda wa siku tisini (90) kuanzia tarehe 06 Septemba, 2025 Leseni ya Huduma za Maudhui Mtandaoni iliyotolewa kwa kampuni ya Vapper Tech Limited (JamiiForums) na kuzuia upatikanaji wa jukwaa la JamiiForums.

Imetolewa tarehe **06 Septemba, 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Sat Sep 06 13:34:17 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz